UHURU UK 5

65> Ni asilimia za mchango wa sekta ya kilimo kwa malig

# Mwigulu ataka wakulima, wafugaji kupata mikopo

Na MWANDISHI WETU, *Arusha*

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameiagiza Menejimenti ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), iweke masharti nafuu ya mikopo, kuwezesha wakulima, wavuvi na wafugaji kupata mikopo hiyo kwa urahisi.

Dk. Nchemba alitoa agizo hilo jijini Arusha jana alipozindua Ofisi ya Kanda ya Kaskazini ya benki hiyo, itakayohudumia mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga.

"Aidha, Maofisa Biashara wa Benki wekeni utaratibu wa kuwatembelea wakulima na kuona maendeleo ya miradi yao mara kwa mara, kwa kufanya hivyo mtasimamia vizuri fedha zitakazotolewa na kuweza kuleta marejesho na faida kwa benki,"alisema.

Pia, aliagiza menejimenti ya benki hiyo kuweka utaratibu wa kujitangaza na kutangaza fursa za mikopo wanayoitoa kwa wakulima na wafugaji kuzitumia kwa wakati na kwa tija, pia kutoa elimu kuhusu usimamizi wa mipoko kwa wakulima watakaokopeshwa.

Alitoa wito kwa wakazi wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga kuchangamkia fursa ya uwepo wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) Arusha, kupata uelewa zaidi wa utaratibu wa kupata mikopo ya pembejeo bora na zana za kisasa za kilimo wapate tija kupitia kilimo.

Dk. Nchemba aliwataka wanufaika wote wa mikopo kutoka TADB katika kanda hiyo, kufanya matumizi sahihi ya fedha watakazokopeshwa kuendeleza miradi ambayo imeombewa fedha hizo katika mchanganuo wa maombi ya mikopo hiyo.

Akizungumzia kuhusu jitihada za serikali katika kukuza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, Dk. Nchemba, alisema imeongezea bajeti Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kuwa; katika Bajeti ya Mwaka 2023/2024, kupitia Wizara ya Kilimo, Serikali imetenga jumla ya sh. bilioni 970.8 , ikiwa ni ongezeko la asilimia 29.2 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

Kwa upande wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema serikali imetenga jumla ya sh. bilioni 292.5, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 , sekta ya mifugo imetengewa sh.bilioni 112.1 na uvuvi imepangiwa kutumia sh. bilioni 180.5.

"Matarajio ya serikali ni kwamba, jumla ya shilingi trilioni 1.2, ambazo tuliziidhinisha katika wizara hizo mbili zitakwenda kuchochea kilimo, uvuvi na ufugaji wa kisasa, pamoja na kuongeza fursa za ajira na kipato katika mnyororo wa thamani wa sekta hizo tatu na kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa,"alisema.

Alisema kwa mujibu wa takwimu zilizopo, sekta ya kilimo inatoa ajira kwa wastani wa asilimia 75 ya Watanzania wote, inachangia asilimia 100 ya chakula kinachozalishwa nchini, zaidi ya asilimia 65 ya malighafi viwandani, inachangia robo ya Pato la Taifa na robo tatu ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

MWENYEKITI WA BODI

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TADB, Ishmael Kasekwa, alisema katika kuleta matokeo chanya, Bodi ya Wakurugenzi wa TADB imeisimamia kwa weledi na uzalendo Benki ya TADB kuhakikisha malengo kusudiwa kwa serikali na wakulima yanafikiwa.

Alisema licha ya kuwa, TADB ni changa katika soko la biashara ya mabenki, kwa muda mfupi imekuwa na ukuaji endelevu na faida, ambayo katika mwaka 2021, ilipata faida ghafi ya sh. bilioni 16 na mwaka 2022 sh. bilioni 15.6

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema TADB ina Ofisi saba ambazo zipo Kanda ya Ziwa katika Mkoa wa Mwanza, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mkoani Mbeya, Kanda ya Mashariki mkoani Dar es salaam, Kanda ya Magharibi mkoani Tabora, Kanda ya Kati mkoani Dodoma, Kanda ya Kusini mkoani Mtwara na hivi sasa Kanda ya Kaskazini, yenye ofisi Jijini Arusha.

UZINDUZI

la Ngaya.

kondakata wa basi hilo,

HABARI LEO UK 7

# *TADB kukopesha wavuvi bila riba*

Na Deogratias Kishombo, Arusha

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) itaanza kutoa mikopo isiyo na riba kwa wavuvi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege alisema hayo Arusha jana wakati wa uzinduzi wa ofisi za benki hiyo Kanda ya Kaskazini.

Waziri wa Fedha, Dk Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega walihudhuria uzinduzi huo.

"TADB ni benki ya kimkakati kuanzia kwenye kilimo tunatoa mikopo ya chini ya asilimia 10 hivyo tumejipanga kuhakikisha tunaanza kutoa mikopo ya asilimia sifuri kwenye uvuvi," alisema Nyabundege.

Alisema hivi sasa TADB inatekeleza agizo la serikali la kukuza uchumi wa nchi na inatarajia kuongeza mtaji wake kufikia trilioni moja.

"Hivi karibuni tulizindua mpango mkakati wa kutoa fursa kwa sekta za kimkakati na kwa kushirikiana na wizara kuna pia mikopo ya vijana na wanawake," alisema Nyabundege.

Aidha, alisema TADB imeendelea kutoa mikopo kwa viwanda vinavyoongeza mnyororo wa thamani kwa mazao ya kilimo.

"Mpaka hivi sasa tumetoa bilioni 484 kwa viwanda vinavyozalisha mafuta, sukari, kahawa na pamba nchini," alisema Nyabundege.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ulega alisema ili kusaidia sekta ya uzalishaji nchini lazima pawe na mazingira mazuri ya kukopeshwa kwa kuwepo kwa riba nafuu.

"Rais amefungua milango kuna mahitaji makubwa sasa katika ufugaji na uvuvi. Kwa mfano katika mifugo kuna fursa ya kunenepesha ng'ombe kwa ajili ya nyama na maziwa," alisema.

Ulega alisema wanahitaji kuongeza uzalishaji wa maziwa hivyo taasisi za fedha zikipeleka mitaji huko kwa wafugaji uchumi utakua.

CamScanner

ya kuahirishwa maadhimisho hayo.

Profesa Ndalichako

HABARI LEO UK.7

# TADB kukopesha wavuvi bila riba

**Na Deogratias Kishombo, Arusha**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) itaanza kutoa mikopo isiyo na riba kwa wavuvi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege alisema hayo Arusha jana wakati wa uzinduzi wa ofisi za benki hiyo Kanda ya Kaskazini.

Waziri wa Fedha, Dk Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega walihudhuria uzinduzi huo.

"TADB ni benki ya kimkakati kuanzia kwenye kilimo tunatoa mikopo ya chini ya asilimia 10 hivyo tumejipanga kuhakikisha tunaanza kutoa mikopo ya asilimia sifuri kwenye uvuvi," alisema Nyabundege.

Alisema hivi sasa TADB inatekeleza agizo la serikali la kukuza uchumi wa nchi na inatarajia kuongeza mtaji wake kufikia trilioni moja.

"Hivi karibuni tulizindua mpango mkakati wa kutoa fursa kwa sekta za kimkakati na kwa kushirikiana na wizara kuna pia mikopo ya vijana na wanawake," alisema Nyabundege.

Aidha, alisema TADB imeendelea kutoa mikopo kwa viwanda vinavyoongeza mnyororo wa thamani kwa mazao ya kilimo.

CamScanner

has invested some 25 million US dollars (62.5bn/) to establish an assembling

out of the plant mid-next March.

The Saturn Corporation

in full swing.

"We are expecting to produce 10 tractor trucks

The CEO said that the plan is to pass the skills to the locals and after two

Kigamboni industrial

DAILY NEWS PAGE 15




*MINISTER for Finance, Dr Mwigulu Nchemba cuts a ribbon to launch Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) Northen Zone Branch in Arusha Region yesterday. Third right is Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega, TADB Board Chairman, Ishmael Kasekwa (second left), Banks Managing Director, Frank Nyabundege (fourth right) and other officials. (Photo courtesy of Ministry)*